



TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI APRILI, 2025

11.04.2025, Dodoma.

Wahitimu wote wa kada za Uuguzi, Ukunga na Utaalamu wa dawa za usingizi na ganzi, wanaotarajia kufanya Mtihani wa Usajili na Leseni, mnatangaziwa kuwa dirisha la maombi litafunguliwa rasmi kuanzia **Jumamosi ya tarehe 12.04.2025 hadi Jumatatu ya tarehe 12.05.2025.**

Maombi yatafanyika kwa njia ya mtandao kwa kutumia mfumo Rasmi wa Baraza <https://tnmcis.tnmc.go.tz/> muombaji kwa mara ya kwanza anatakiwa kujisajili na kulipia kiasi cha **Tsh. 150,000/=** na muombaji anayerudia atalipia kiasi cha **Tsh. 75,000/=**

Aidha, Mtihani unatarajiwa kufanyika **tarehe 23.05.2025** hivyo kila muombaji anatakiwa kuzingatia taratibu zote za maombi kama ifuatavyo :-

- Uwe umefaulu Mtihani wa kufuzu Mafunzo kwa Ngazi husika (*Qualifying Examination*),
- Uwe na namba ya utambulisho (*Indexing Number*) kwa mujibu wa kifungu cha 14 (01) cha kanuni za mafunzo,
- Kuweka picha sahihi (*Passport Size 45mmX35mm*) background iwe ya *Lightblue*,
- Kujaza majina sahihi yanayoendana na vyeti vya kumaliza Elimu ya Sekondari,
- Kufanya malipo na kuchagua kituo sahihi cha Mtihani kwa wakati

ORODHA YA VITUO VYA MTIHANI

S/N	KITUO CHA MTIHANI	MKOA	IDADI
01	CHUO KIKUU CHA ST.JOHN'S	DODOMA	700
02	CHUO KIKUU CHA KAMPALA	DAR ES SALAAM	900
03	TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI- TANDABUI	MWANZA	900

Imetolewa na:

Agness Mtawa
MSAJILI TNMC